

## **TAARIFA KWA WANACHAMA WOTE WA TASTA KUHUSU MKUTANO MKUU WA CHAMA**

Ndugu Wanachama, kamati tendaji ya chama ilifanya kikao chake cha kawaida kwa mujibu wa Katiba ya chama ibara ya 28(a) tarehe 14/02/2022 na kuongozwa na Mwenyekiti Ndugu Titus Mwisomba. Kikao kilijadili mambo mbalimbali yanayohusu chama. Pamoja na mambo mengine kamati iliazimia mambo yafuatayo;

1. Kufanyike Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanachama tarehe 20/10/2022 katika jiji la Arusha. Mkutano Mkuu wa Chama utafanyika kwa mujibu wa katiba ya Chama ibara ya 25(a). Mkutano huu pamoja na mambo mengine utajadili shughuli mbalimbali zilizofanywa na chama, kujadili na kupitisha shughuli za chama kwa mwaka 2022/2023.
2. Kufanyika kongamano la Kitakwimu tarehe 18 na 19 Oktoba 2022 katika jiji la Arusha. Lengo la kongamano ni kuwakusanya watakwimu kote nchini na hata nje ya nchi ili kujifunza na kubadilishana mawazo kupitia mada zitakazowasilishwa wakati wa kongamano. Mada ya kongamano ni “Takwimu Sahihi kwa Maendeleo ya Taifa”. Wanachama wote wanaalikwa kuwasilisha ikisiri kwa ajili ya kutathiminiwa kabla ya kupitishwa na kuwasilishwa siku ya kongamano.

**IMETOLEWA NA OFISI YA KATIBU  
CHAMA CHA WATAKWIMU TANZANIA (TASTA)  
01/03/2022**